TANGAZO LA SERIKALI Na. 8 La Tarehe 13/1/2023

SHERIA YA MASHIRIKA YA UMMA,

(SURA YA 257)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 38(3))*

AMRI YA KUTAMKA MASHIRIKA YA UMMA KUTOKUWA CHINI YA UANGALIZI YA MWAKA 2023

KWA KUWA, Msajili wa Hazina katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa kifungu cha 22 cha Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya 257 ametoa mapendekezo kwa Waziri wa Fedha kwamba baadhi ya Mashirika ya Umma kutamkwa kuwa yameondolewa kutoka kuwa chini ya uangalizi;

NA KWA KUWA, kupitia kifungu cha 38(1) cha Sheria hiyo, Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha alitamka mashirika ya umma mbalimbali kuwa chini ya uangalizi kupitia matangazo mbalimbali ya Serikali kama ilivyoainishwa katika Jedwali; na

NA KWA KUWA, kifungu cha 38(3) cha Sheria hiyo kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha, kwa Amri iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali, kuweza kurekebisha, kubadilisha au kurudisha Amri yoyote iliyotolewa chini ya kifungu hiki;

HIVYO BASI, Mimi MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU, Waziri wa Fedha na Mipango, katika kutekeleza mamlaka niliyopewa na kifungu cha 38(3) cha Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya 257, natoa Amri ifuatayo:

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutamka Mashirika ya Umma Kutokuwa Chini ya Uangalizi ya Mwaka 2023.

Tamko la mashrika ya umma

2. Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika Jedwali yanatamkwa kuwa yameondolewa kutoka kuwa chini ya

kutokuwa chini ya uangalizi Sura ya 257

uangalizi na masharti ya Sheria ya Mashirika ya Umma, yatatumika kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa Amri hii.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Jina la Shirika | Tangazo la Serikali |
|---|---|---|
| 1. | Mkata Sawmills Limited | T.S Na.23 la mwaka 1995 |
| 2. | Polysacks Company Limited | T.S Na. 400 la mwaka 1995 |
| 3. | Sikh Sawmills Limited | T.S Na.324 la mwaka1996 |
| 4. | Mang'ula Mechanical and Machine Tools Limited | T.S Na.33 la mwaka1997 |

Dodoma,
30 Desemba, 2022

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha na Mipango*